**TAARIFA KWA UMMA**

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA URATIBU WA MILIKI UBUNIFU KATIKA MIAKA 60 YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR**

**Dar es Salaam-24 Aprili, 2024**

Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA) kwa kushirikiana na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) imekuwa na mafanikio makubwa kwenye eneo la Miliki Ubunifu kwa kipindi cha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kupitia Taasisi hizi zinazosimamia Miliki Ubunifu kwa upande wa Tanzania Bara (BRELA) na kwa upande wa Zanzibar (BPRA) mafanikio yaliyopatikana yamegawanyika katika ngazi tatu; Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

**Kitaifa.**

i. Mashirikiano mazuri na ya karibu katika ubadilishanaji wa taarifa, kushirikishana ujuzi na uzoefu baina ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA). Ushirikiano huu umeziwezesha Taasisi hizi mbili kupiga hatua kubwa kwenye utendaji kazi wake kama Wakala za Serikali, lengo likiwa ni kutoa huduma kwa uharaka, ubora, weledi na ufanisi.

ii. Mashirikiano hayo yamezifanya Taasisi hizi mbili kuwa na mifumo inayofanana katia uchakataji na ushughulikiaji wa maombi ya Alama za Biashara na Huduma pamoja na Hataza. Mifumo hii ya kielektroniki inajulikana kama, Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (Online Registration System - ORS) pamoja na mfumo wa kuchakata na kuhifadhi maombi ya Miliki Ubunifu (Intellectual Property Automated System (IPAS)).

**Kikanda**

Mwaka 1976, Tanzania ilijiunga na Shirika la Miliki Ubunifu la Kanda ya Afrika (African Regional Intellectual Property Organization-ARIPO). Kupitia ARIPO nchi imesaini na kuridhia Itifaki katika Usimamizi wa Maeneo Mahsusi ya Miliki Ubunifu, Itifaki hizo na manufaa yaliyopatikana ni kama ifuatavyo;

i. Mwaka 1982, Tanzania ilisaini na kuridhia Itifaki ya Harare ya Ulinzi wa Hataza na Maumbo Bunifu (Harare Protocol on Protection of Patents and Designs) imewezesha wabunifu kulinda bunifu zao ikiwa ni Hataza na Maumbo Ubunifu kupitia ARIPO hivyo kuongeza wigo wa ulinzi wa bunifu husika.

ii. Mwaka 1993, Tanzania ilisaini Itifaki ya Banjul ya Ulinzi wa Alama (Banjul Protocol on the Protection of Marks 1993), Itifaki hii inatoa fursa kwa Wabunifu wa Alama (nembo) kusajili na kupata ulinzi wa Alama za Biashara na Huduma kwa kupitia ARIPO hivyo kuongeza wigo wa ulinzi kwa Wabunifu husika.

iii. Mwaka 2015 Tanzania ilisaini Itifaki ya Arusha ya Ulinzi wa Mbegu Mpya za Mimea, itifaki hii inatoa fursa kuongeza wigo wa ulinzi kwa Wagunduzi wa aina mpya za Mbegu za mimea.

iv. Mwaka 2021 Tanzania ilisaini Itifaki ya Kampala ya Usajili wa Hiyari wa Hakimiliki na Hakishiriki.Itifaki hii inatoa fursa kuongeza wigo wa ulinzi wa Wabunifu wa kazi za sanaa na uandishi.

v. Mwaka 2023 Tanzania ilisaini Itifaki ya Ulinzi wa Haki za Miliki Ubunifu chini ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (Protocol on Protection of Intellectual Property Rights under the African Continental Free Trade Area - AfCFTA).

Kwa kuwa mwanachama wa Shirika hili nchi imenufaika katika mambo mbalimbali;

- Kujengewa uwezo na kuongeza ujuzi na utaalam katika eneo la Miliki Ubunifu na kujifunza kutoka Nchi nyingine Wanachama,
- Kutoa elimu kwa kuanzisha Shahada ya Umahiri katika Miliki Ubunifu inayotolewa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**Kimataifa**

Mwaka 1983, Tanzania ilijiunga na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (World Intellectual Property Organization – WIPO) kupitia Mkataba wa Stockholm, uanachama wa Tanzania WIPO, imeifanikisha nchi kujiunga na Mikataba inayohusiana na Usimamizi na uratibu wa masuala mbalimbali yanayohusu Miliki Ubunifu kama ifuatavyo:-

i. Mkataba Paris wa Ulinzi wa Mali Ubunifu (Paris Convention for Protection of Industrial Property of 1883)
ii. Mkataba wa Berne wa ulinzi wa Kazi za Uandishi na Sanaa (The Berne Convention for the Protection of Literary and Artistic Works of 1886),
iii. Mkataba wa Nice wa Madaraja ya Alama za Biashara na Huduma (Nice Agreement concerning the International Classification of Goods and Services of 1957).
iv. Mkataba wa Ushirikiano wa Hataza (The Patents Cooperation Treaty (PCT) of 1970).
v. Katika masuala ya ulinzi wa hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (International Convention for the Protection of New Varieties of Plants chini ya International Union for the Protection of New Varieties of Plants)

Pia Tanzania imejiunga uanachama na Shirika la Biashara Dunia (WTO) kupitia uanachama nchi inatakiwa kutekeleza Mkataba wa Masuala ya Miliki Ubunifu yanayohusiana na Biashara wa mwaka 1994 (Trade-Related Aspects of Intellectual Property Agreement (TRIPS) of 1994 of the World Trade Organization).

Mkataba huu unatoa nafuu na fursa katika eneo la Miliki Ubunifu ambazo ni pamoja na uwezekano wa kutumia teknolojia za dawa na vifaa tiba ambazo zinapatikana katika Hataza (Patent). Hii inawezesha upatikanaji rahisi wa dawa

na vifaa tiba kwa bei nafuu au kutumia teknolojia hizo pasipo kupata matatizo ya Kisheria kutoka kwa wamiliki wa teknolojia husika.

Hivyo, kupitia uanachama wa nchi katika Mikataba hii ya Kikanda na Kimataifa ya uratibu na usimamizi wa Miliki Ubunifu, nchi imenufaika kama katika kuongeza ujuzi kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu, uhawilishaji wa teknolojia, kubadilishana ujuzi katika masuala ya Miliki Ubunifu na kuwezesha kuongeza wataalam wa Miliki Ubunifu nchini, kukuza uelewa wa matumizi ya Miliki Ubunifu kwa maendeleo endelevu na kuboresha mifumo ya Usimamizi na uratibu wa Miliki Ubunifu kwa pande zote mbili za Muungano.

Imetolewa na;

**Kitengo cha Uhusiano**